MINISTRY OF HEALTH

MASWALI AMBAYO HUULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU CHANJO YA UGONJWA WA COVID-19 NCHINI KENYA

Sehemu hii inatoa maelezo na majibu ya hivi punde kwa maswali ya wananchi kuhusu chanjo ya COVID-19 nchini Kenya. Majibu haya yanalenga kutoa habari sahihi, za kuaminika na kwa wakati ufaao kwa umma kuhusu shughuli inayoendelea ya utoaji chanjo ya COVID-19 katika taifa la Kenya. Waraka huu hupigwa msasa mara kwa mara ili kujumuisha matukio na masuala ibuka.

Kwa habari zaidi, piga simu kwa nambari maalum ya moja kwa moja ya Wizara ya Afya kuhusiana na COVID-19 ya 719.

Swali	Jibu
COVID-19 inamaanisha nini?	COVID-19 inamaanisha ugonjwa wa virusi vya corona wa mwaka 2019. Ni jina rasmi lililotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona vya SARS-CoV2. Kirusi SARS-CoV2 ni kirusi kipya ambacho hakijawahi kuonekana hapo awali kwa wanadamu. Hii inamaanisha ni tofauti na virusi vya corona ambavyo husababisha homa ya kawaida, na vile vilivyosababisha ugonjwa wa SARS mwaka 2002 na MERS mwaka 2012. Visa vya kwanza vya virusi vya SARS-CoV2 viliripotiwa Desemba 2019. WHO ilitambua rasmi ugonjwa huu kama COVID-19 katika taarifa kwa vyombo vya habari mnamo Februari 11, 2020.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Je, COVID-19 ni sawa na homa ya kawaida?	La, COVID-19 na homa ya kawaida sio sawa. COVID-19 husababishwa na virusi geni vya SARS-CoV2 ambavyo havijawahi kuonekana kwa wanadamu. Homa na mafua husababishwa na aina tofauti za virusi ambavyo humpata binadamu kwa kawaida. Tofauti na homa, COVID-19 wakati mwingine humfanya mtu kupoteza ghafla uwezo wake wa kunusa na kuonja. Idadi ya watu ambao wako hatarini kulemewa mno au kufa kutokana na COVID-19 ni hadi mara 10 zaidi ikilinganishwa na homa ya kawaida au mafua.
Kwa nini COVID-19 inatambuliwa kama janga?	Mnamo Machi 11, 2020, WHO iliiratibisha rasmi COVID-19 kama janga. Janga ni mlipuko wa ugonjwa kote duniani ambao huenea kwa haraka katika mataifa na mabara mbalimbali. WHO iliamua kuratibisha COVID-19 kama janga kuambatana na vigezo vifuatavyo: •Katika kipindi cha wiki mbili tu, idadi ya visa vya COVID-19 nje ya China vilikuwa vimeongezeka mara 13. • Idadi ya mataifa yaliyoathiriwa ilikuwa mara tatu. • Kulikuwa na zaidi ya visa 118,000 katika mataifa 114. • Watu 4,291 walikuwa wameaga dunia. • Maelfu zaidi walikuwa wamelazwa hospitalini. COVID-19 ndio virusi vya kwanza vya corona kuratibishwa kama janga. Hii inatokana na idadi kubwa ya vifo na msambao wa haraka wa ugonjwa huo.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Je, serikali ina mpango gani wa chanjo dhidi ya COVID-19 nchini Kenya?	Serikali ya Kenya imedhamiria kutoa chanjo kwa watu wote wazima (miaka 18 na zaidi) wanaoishi nchini Kenya ifikapo Juni 2022. Chanjo ya COVID-19 itatolewa kwa awamu tatu. Awamu hizo sio za kipekee na zinaweza kuingiliana. **Awamu ya 1:** Hii ilianza Machi 2021 na ililenga watu walio 'mstari wa mbele' katika vita vya kupambana na COVID-19. Hawa ni pamoja na wahudumu wa afya; walimu na wafanyakazi katika taasisi zote za elimu; maafisa wa usalama – polisi, wanajeshi, maafisa wa magereza; maafisa wa uhamiaji; wakufunzi katika taasisi za kidini na watu wenye umri wa miaka 58 na zaidi. **Awamu ya 2:** Hii inaendelea na inalenga wahudumu walio mstari wa mbele kupambana na janga hili, pamoja na watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi hususan wale ambao tayari wanaugua maradhi sugu. **Awamu ya 3:** Hii italenga watu wote wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi. **Wale ambao tayari wanaugua maradhi mengine wanahimizwa kupata chanjo.**
Ni wakati gani nitarajie kupokea chanjo yangu ya COVID-19?	Serikali ya Kenya ilianza kutoa dozi ya kwanza ya chanjo ya AstraZeneca/Covishield mwezi Machi 2021. Serikali pia inataka kuhakikisha wale wote waliopokea dozi hiyo ya kwanza wanapata pia ya pili ili kuimarisha idadi ya wananchi ambao wamepata chanjo kamili nchini.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Naweza kupata wapi habari sahihi kuhusu chanjo ya COVID-19 na shughuli ya utoaji chanjo nchini Kenya?	Kwa habari sahihi na za kuaminika kuhusu chanjo dhidi ya COVID-19, tafadhali tembelea tovuti ya Wizara ya Afya https://www.health.go.ke au piga simu kwa nambari maalum ya Wizara kuhusiana na COVID-19 ya 719 au bonyeza *719# Unaweza pia kutembelea tovuti za Shirika la Afya Duniani (WHO) au Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Watoto (UNICEF) kupata habari sahihi kuhusu chanjo na shughuli ya utoaji chanjo.
Ni chanjo zipi za COVID-19 ambazo Wizara ya Afya imeidhinisha kutolewa Kenya?	Chanjo ndio mkakati mkuu ambao umetambuliwa kama njia ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 pamoja na hatua nyingine za kuzuia maambukizi. Shirika la Afya Duniani limeidhinisha na kupendekeza chanjo nyingi dhidi ya COVID-19. Wizara ya Afya iliidhinisha matumizi ya chanjo ya **AstraZeneca /Covishield** nchini katika mpango wake wa awali wa kinga. Wizara sasa pia imeidhinisha chanjo za **Pfizer, Moderna, Sinopharm** na **Johnson &Johnson.**
ANi dozi ngapi za chanjo ya COVID-19 nahitaji kupokea na kwa kipindi kipi?	Idadi ya dozi unazopokea inategemea aina ya chanjo ya Covid 19 ambayo umepewa. AstraZeneca/Covishield, Pfizer, Moderna na Sinopharm ni chanjo za dozi mbili. Hii inamaanisha utahitaji kupewa dozi mbili kwa vipindi vya kati ya wiki 4 - 12 kama ionavyopendekezwa na WHO ili kupata kinga kamili. Chanjo ya Johnson &Johnson COVID-19 inahitaji dozi moja pekee kwa kinga kamili.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Nini kitatokea iwapo nitakosa kupata dozi ya pili ya chanjo ya COVID-19 kwa wakati unaofaa?	Unashauriwa kupokea dozi zote mbili ili kupata kinga kamili kwa chanjo za dozi mbili. Iwapo kwa sababu fulani utakosa kupokea dozi yako ya pili katika kipindi kilichopendekezwa, unashauriwa kutembelea kituo cha afya kilicho karibu nawe haraka iwezekanavyo ili kupata dozi ya pili.
AKwa nini chanjo ya COVID-19 inahitajika ilhali kuna hatua zingine za afya ya umma za kuzuia maambukizi kama vile kutengana kimwili, kuvaa barakoa na kuosha mikono?	COVID-19 haina tiba. Kuzima msambao wa janga la COVID-19 kutahitaji hatua kadhaa ambazo pia zinajumuisha chanjo ya Covid 19. Chanjo hupiga jeki kinga yako ya mwili na kukuandaa kupambana na virusi iwapo utaambukizwa. Wizara ya Afya inahimiza wananchi kuendelea kutekeleza kanuni hizo za kuzuia maambukizi ambazo ni pamoja na; • Kutumia sanitaiza yenye kileo ama kunawa mikono kwa maji na sabuni mara kwa mara. • Kuvaa barakoa ukiwa nje ama palipo na mikusanyiko ya watu. • Kutengana kimwili angalau mita 1.5 kutoka mtu mwingine. Kupokea chanjo kamili dhidi ya COVID-19 na kufuata kanuni za kuzuia maambukizi ndiyo njia bora zaidi ya kukukinga wewe na walio karibu nawe.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Chanjo za COVID-19 zinafanya kazi vipi?	Chanjo huandaa kinga yako ya mwili kutambua na kupambana na virusi vinavyosababisha COVID-19. Chanjo zimeundwa kufunza kinga ya mwili kubaini na kuangamiza kwa njia salama virusi vinavyosababisha COVID-19. Chanjo ya COVID-19 hutumia kirusi cha corona ambacho kimefanywa bwete au kufifishwa, na hivyo hakisababishi ugonjwa lakini bado kitazuzua kinga ya mwili.
Je, chanjo za COVID-19 ni salama?	Ndio. Chanjo zote za COVID-19 zilizoidhinishwa na kupendekezwa ni salama na zinafanya kazi vyema. Hii ni baada ya kufanyiwa utafiti madhubuti na wa kina. Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya Wizara ya Afya ya https://www.health.go.ke au piga simu kwa nambari maalum ya Wizara kuhusu COVID-19 ya 719 ama bonyeza *719#.
Ni nani anastahili kupata chanjo ya COVID-19?	Watu wote wazima walio na umri wa zaidi ya miaka 18 wanakubaliwa kupata chanjo ya COVID-19. Hata hivyo, kipaumbele kinapewa watu walio na afya iliyodhoofika, wahudumu walio mstari wa mbele kupambana na janga hili na wakongwe.
Ni nani ambaye hafai kupata chanjo ya COVID-19?	Chanjo kwa sasa **HAIPEWI**; 1. Watoto 2. Yeyote anayeathiriwa na mzio wa chanjo nzima au baadhi ya viungo vya chanjo. 3. Yeyote aliye na dalili za mafua/COVID-19 wakati anapojiwasilisha kupata chanjo. Wanawake wajawazito wanaweza kuchanjwa kulingana na hali ya kila mmoja iwapo atakaguliwa na kupatikana kuwa katika hatari kubwa ya kuugua makali ya COVID-19.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Je, chanjo ya COVID-19 husababisha madhara?	Baadhi ya chanjo za COVID-19 zina madhara, hii ikiwa ni dalili za kawaida kwamba mwili wako unaandaa kinga. Miongoni mwa dalili hizi zinazoweza kushuhudiwa ni pamoja na: uchungu na uvimbe kwenye mkono ulipodungwa sindano ya chanjo, homa, kijibaridi, uchovu na maumivu ya kichwa. Madhara haya kwa kawaida yanafaa kukoma baada ya siku chache. Wizara ya Afya inathibitisha kwamba manufaa ya chanjo ya COVID-19 yanazidi hatari zinazoweza kukupata. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu madhara ya chanjo za COVID-19 kwenye tovuti https://www.pharmacyboardkenya.org/blog/2021/03/pvers-ii-launch
Je, chanjo ni salama kwa watu wenye maradhi sugu na magonjwa ya moyo?	Ndio, wagonjwa wa moyo au kisukari ni miongoni mwa makundi yaliyopewa kipaumbele kupokea chanjo dhidi ya COVID-19. Aina zote za chanjo ya COVID-19 ni salama kwao.
Je, kuna mtu yeyote amefariki kutokana na chanjo ya COVID-19?	La. Hakuna vifo vilivyoripotiwa kutokana na chanjo ya COVID-19 nchini Kenya. Wizara ya Afya kupitia Halmashauri ya Dawa na Bidhaa za Sumu (PPB) hukusanya taarifa kila siku kuhusu Matukio Mabaya Yanayotokana na Utoaji Chanjo (AEFI) ambayo yamesababishwa na chanjo ya COVID-19 nchini Kenya. Ikiwa una habari zozote za AEFI kufuatia utoaji chanjo ya COVID-19 nchini Kenya, tafadhali piga simu kwa nambari mahususi ya Wizara kuhusu COVID-19 ya 719 au ripoti kupitia mtandaoni kwa anwani https://pv.pharmacyboardkenya.org/padrs/add

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Kwa nini nahitaji kupata chanjo dhidi ya COVID-19?	Chanjo ya COVID-19 husaidia kuzuia makali na kifo kutokana na ugonjwa huu. Faida zingine ni pamoja na; **Kinga kwako na jamii** • Unapopata chanjo, unajikinga mwenyewe na kusaidia kukinga jamii nzima. • COVID-19 inaweza kuenea haraka na kwa kiwango kikubwa. Imesababisha vifo vya zaidi ya watu milioni 4.4 duniani na zaidi ya vifo 4,000 nchini Kenya. • Idadi ya kutosha ya watu katika jamii wanapochanjwa, itapunguza kasi ya msambao wa ugonjwa. **Kupunguza athari za kiuchumi za janga la COVID-19** • Viwango vya juu vya chanjo hupunguza uwezekano wa milipuko kutokea. Hii nayo huondoa haja ya kuwepo kwa kanuni kali za kuzuia maambukizi kama vile kafyu, amri za kutotoka nje kabisa na udhibiti wa matembezi. • Matokeo yake ni kwamba chanjo itaokoa maisha na kulinda shughuli za kutegauchumi.
Nitawezaje kuamua aina ya chanjo ya COVID-19 nitakayopokea?	Chanjo zote zilizoidhinishwa na kupendekezwa za COVID-19 ni salama, utendakazi mwafaka na zinatolewa bila malipo. Wizara ya Afya haipendekezi aina moja ya chanjo dhidi ya nyingine. Chanjo zote hutoa kinga kamili mwilini ikiwa utapokea dozi zote zilizopendekezwa. Jambo la muhimu zaidi ni wewe kupata chanjo ya COVID-19 haraka iwezekanavyo kutoka kituo cha afya kiliko karibu nawe. Idadi kubwa kabisa ya wananchi inapochanjwa ndiyo silaha muhimu katika vita vya kuzima janga hili.

unicef

World Health Organization

Je, nawezaje kuchanganya chanjo? Iwapo nilipokea dozi ya kwanza ya AstraZeneca/ Covishield naweza kupata dozi ya pili ya aina nyingine ya chanjo?	Shirika la Afya Duniani (WHO) limetoa mwongozo kuhusu suala la kuchanganya chanjo iwapo kutakuwa na uhaba wa chanjo ya COVID-19. Kwa sasa nchini Kenya, suala la kuchanja chanjo za COVID-19 halijaruhusiwa kama sera. Hata hivyo, suala hili linazidi kupigwa darubini na maagizo kutolewa inapohitajika.
Je, ninaweza kupata wapi chanjo dhidi ya ugonjwa wa COVID-19?	Serikali ya Kenya imechukua hatua mwafaka kuwasilisha chanjo za COVID-19 kwa watu wote wanaoishi nchini Kenya, ikiwemo wakimbizi na wahamiaji, kwa misingi ya sera ya usawa na upatikanaji sawa. Chanjo zote zitatolewa katika vituo vya chanjo ambavyo vimeidhinishwa na Wizara ya Afya. Orodha rasmi ya vituo hivyo inapatikana kwenye tovuti ya wizara https://www.health.go.ke au piga simu kwa nambari maalum ya Wizara kuhusu COVID-19 ya 719. **Chanjo ya COVID-19 inatolewa bila malipo.**
Je, nahitaji kujisajili ili kupokea chanjo dhidi ya ugonjwa wa COVID-19?	Ndio, kusajiliwa au kuandikishwa kwenye sajili ya kidijitali ya CHANJO inahitajika kwa yeyote kupokea chanjo ya COVID-19. Hii inatoa fursa ya ufuatiliaji mzuri wa watu ambao wamepokea chanjo na pia utoaji sahihi wa Vyeti kwa waliopokea chanjo kikamilifu. Jisajili kupitia tovuti ya Wizara ya Afya portal.health.go
AJe, watoto wanaweza kuchanjwa dhidi ya COVID-19?	La. Kwa sasa hakuna mtu chini ya umri wa miaka 18 anayestahili kupata chanjo hiyo. Watoto hawapatwi na makali ya ugonjwa wa COVID-19. Hata hivyo, hili linaweza kubadilika kadri habari zaidi kuhusu chanjo zinapatikana.

unicef

World Health Organization

MINISTRY OF HEALTH

Je, naweza kuacha kufuata maagizo yote ya kuzuia COVID-19 baada ya kupata chanjo kamilifu?	Hapana, Wizara ya Afya inapendekeza kwamba kila mtu, ikiwemo wale ambao wamechanjwa kikamilifu, aendelee kuzingatia masharti na kanuni zote zilizopo za kuzuia maambukizi ya COVID-19, kama vile kujitenga kimwili na wengine, kuepuka mikusanyiko ya watu, kuvaa maski na kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji au kutumia sanitaiza yenye kileo. Hii itakupa ulinzi bora zaidi dhidi ya kuambukizwa na kueneza ugonjwa wa COVID-19.
Je, naweza kuambukizwa COVID-19 hata baada ya kupata chanjo?	Licha ya chanjo ya COVID-19 kuwa na ufanisi mkubwa wa kinga, haitoi ulinzi wote wa asilimia 100% na hivyo idadi ndogo ya watu bado wataambukizwa ugonjwa huu. Chanjo, hata hivyo, hupunguza pakubwa mno makali na kifo.
Iwapo tayari niliambukizwa COVID-19 na nimeshapona, je, bado nahitaji kupokea chanjo ya COVID-19?	Ndio, mtu anaweza kupokea chanjo ya COVID-19 hata baada ya kuambukizwa ilmradi awe amepona kabisa. Hata hivyo, wale ambao kwa sasa wanaugua COVID-19 wanapaswa kuahirisha shughuli ya kupewa chanjo hadi baada ya ugonjwa huo kupona kabisa; na pia baada ya kutimiza maagizo ya mamlaka za afya ya kujitenga (kukamilisha siku 10 za kuwa katika karantini). Aidha, watu waliopokea matibabu fulani maalum walipokuwa wagonjwa COVID-19 watahitaji kusubiri zaidi kupokea chanjo hadi baada ya kipindi cha siku 90. Pata ushauri wa wahudumu wa afya kufahamu lini unaweza kupokea chanjo yako ya COVID-19.

unicef World Health Organization

Je, kinga hukaa muda gani mwilini baada ya kupata chanjo ya COVID-19?	Watafiti bado hawajajua ni muda gani kinga hudumu mwilini baada ya chanjo. Ndiyo maana unahimizwa kuendelea kufuata masharti ya afya ya kuzuia maambukizi kwa sababu ni muhimu sana.
Ikiwa nitapata chanjo ya COVID-19, je, yaweza kusababisha vipimo vya COVID-19 (PCR au antijeni) kutoa matokeo ya uongo?	Kupokea chanjo ya COVID-19 hakutasababisha vipimo vya PCR au vya antijeni kwenye maabara kuonesha una ugonjwa, kwani vipimo hivi husaka chembechembe zilizo hai wala sio iwapo mtu ana kinga au la.
Je, kuchanjwa dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 ni lazima kwa watu wote wanaoishi Kenya?	Ingawa sio lazima kupata chanjo ya COVID-19, Serikali inawahimiza wale wote wanaostahili kupata wafanye hivyo. Chanjo zinapatikana na zimeidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Wizara ya Afya (MoH). Kupokea chanjo ni muhimu sana kwa Kenya na ulimwengu kwa jumla ili kukabiliana na athari mbaya za ugonjwa za COVID-19 na kulinda maisha ya walio hatarini zaidi. Takwimu pia zinaonyesha kuwa taifa lililo na idadi ya juu ya wananchi waliopokea chanjo hupunguza pakubwa viwango vya maambukizi ya COVID-19.